MTAAL WA UMILISI

SEHEMU YA KWANZA:
KISWAHILI - LUGHA **Muda: Saa**
1 dakika 40

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Kasomi alikuwa mwanafunzi wa darasa la sita. Hakuwa mwerevu sana na pia hakuwa **mjinga kama samaki**. Kwa kweli, hakuna mwanafunzi mjinga sana ambaye hawezi kufunzwa akaelewa. Ukimwona mtoto anashindwa kuelewa masomo darasani, yeye mwenyewe ameamua kwamba hataki
kusoma wala kuelewa. Na ukiona ameamua hivyo, yeye ana mambo mengine kichwani na moyoni ambayo anayashughulikia yakachukua nafasi ya masomo. Kumbuka, huwezi kutumikia vitu viwili kwa wakati
mmoja.
Huwezi kupanda farasi wawili kwa wakati mmoja. Njia mbili zilimshinda hata fisi na ulafi wake. Kasomi alianza kuwa duni darasani. Jambo hili lilinishangaza. Mbona kitambo alikuwa chapuchapu?
Aliuliza maswali na kuyajibu mengine darasani. Maswali haya yalinisumbua mpaka siku moja nikaanza kuchunguza mienendo yake. Nikagundua kuwa yeye hurudi darasani kisirisiri wakati wengine wako uwanjani wakicheza. Humo alipekuapekua mikoba na madawati ya wenzake akachukua vya kuchukua. Alikuwa mwizi! Leo amekamatwa. Aibu! Wizi na masomo, ni kipi bora?

Maswali

1. Kasomi alikuwa mwanafunzi wa
   kiwango gani darasani?
   A. Duni
   B. Wastani
   C. Juu
   D. Mwerevu.

2. Mtoto anayefeli ovyoovyo darasani
   ni yule ambaye
   A. haelewi
   B. hataki kusoma
   C. ameshindwa
   D. ni mjinga.

3. Kasomi hakuwa **mjinga kama samaki** .
   Hii ni tamathali gani ya lugha?